JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE

015 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda : Saa 3 **Mwaka: 2023**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na moja (11)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na B na maswali **mawili (2)** katika sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **kumi na sita (16)**, sehemu B alama **hamsini na nne (54)** na sehemu C ina **alama thelathini (30)**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 301015 100012

SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Maana ya elimu kwa mujibu wa Uislamu inapatikana kwa kuzingatia jambo gani?
A Alama za ufaulu katika vyeti
B Uwezo wa kutambua mazingira
C Aina ya ajira unayoweza kupata
D Ufanisi na ubora wa kivitendo
E Uwezo wa kuchambua na kueleza

(ii) Allah amesema; *"Haitokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika kitabu kabla hatujaumba. Kwa yakini hilo ni sahali kwa Allah"*. Aya hiyo inaeleza kuhusu itikadi gani ya Uislamu?
A Upweke wa Allah (S.W)
B Vitabu vya Allah (S.W)
C Qadar ya Allah (S.W)
D Mitume ya Allah (S.W)
E Malaika wa Allah (S.W)

(iii) Bwana Bakari anajizuia na vyakula vizuri, anavaa nguo chakavu na kuishi katika nyumba isiyo na sakafu, akiamini kuwa kufanya hivyo ni kujinyenyekeza na kujikurubisha zaidi kwa Mungu. Bwana Bakari atakuwa ameathiriwa na mfumo gani wa maisha?
A Uislamu
B Uyahudi
C Ukristo
D Umajusi
E Utawa

(iv) Ibada gani inaingia katika mifano ya *Fiqh-Muamalaat* kati ya ibada zifuatazo;
A Sala
B Mirathi
C Zakat
D Funga
E Hijja

(v) Jambo lipi ni lazima kutekelezwa katika mchakato wa kumuosha maiti?
A Kumfunika shuka maiti gubigubi
B Kuanza na kumuweka maiti udhu
C Kutumia maji ya kisima au mto
D Kutumia kitanda kilichotobolewa
E Kujizuia kuongea wakati wa kuosha

(vi) Kwa nini Maquraysh walipinga kwa nguvu kubwa ujumbe wa Mtume Muhammadi (S.A.W)?
A Walihofia kuharibika kwa maslahi yao ya kimali
B Waliogopa kuharibiwa kwa makanisa yao
C Walihofia mustakbali wa miungu yao ya sanamu
D Walihofia kupoteza ushawishi wa kuhudumia Qa'aba
E Walihofia kufukuzwa katika mji mtakatifu wa Makkah

(vii) Nabii gani alipokea majukumu ya ulinganiaji wa dini ya Allah (S.W) baada ya Yaaqub (A.S)?

A Is-haq (A.S) B Musa (A.S) C Yusuf (A.S)
D Il-yaas (A.S) E Idrisa (A.S)

(viii) Hoja gani inathibitisha usahihi wa Hadithi kwa kuangazia vigezo vya matini?

A Wasimulizi wadhibitifu
B Wingi wa wasimulizi
C Kuandikwa na Bukhar
D Kuwepo kwenye vitabu sita
E Kuwiana na mambo ya hakika

(ix) Qur'an imeshushwa kidogo kidogo kwa sababu mbalimbali zilizo bayana **isipokuwa**

A Kuuthibitisha moyo wa Mtume (S.A.W)
B Kuwapa nafasi wengine kuleta mfano wake
C Kufanya wepesi wa kufika ujumbe wake
D Waumini kupata wepesi wa kuihifadhi
E Kufanya wepesi katika utekelezaji wake

(x) Miongoni mwa Nguzo tano za Uislamu, nguzo ya shahada inasisitiza jambo gani katika maisha ya muumini?

A Kufanya kazi ya kuwatamkisha wengine.
B Kuanza jambo na jina la Allah (S.W) na Mtume (S.A.W).
C Hakuna nabii mwingine isipokuwa Muhammad (S.A.W).
D Kutambua uwepo wa Miungu wengi hapa Duniani.
E Wajibu wa kumtii Allah (S.W) na Mtume (S.A.W).

2. Oanisha nyakati mahususi za Sala kulingana na mwenendo wa jua katika **Orodha A** na majina ya Sala zinazotekelezwa katika nyakati hizo katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kijitabu chako cha kujibia.

Orodha A		Orodha B
(i)	Kuanzia urefu wa kivuli unapokuwa sawa na kitu halisi hadi kivuli kinapokuwa mara dufu ya urefu wa kitu halisi.	A. Dhuha B. Istisqaa
(ii)	Kuanzia mawingu yanapobadilika na kuwa ya njano hadi usiku wa manane.	C. Al-asr D. Dhuhr
(iii)	Baada ya jua kugeuka upande wa magharibi hadi pale urefu wa kivuli unapokuwa sawa na kitu halisi.	E. Al-fajr F. Maghrib
(iv)	Kuanzia pale ambapo alama ya mstari mweupe inapojitokeza upande wa mashariki hadi mwangaza unapodhihiri.	G. Al-Ishaa H. Qusufi
(v)	Kuanzia jua linapozama hadi pale mawingu mekundu yanapobadilika na kuwa ya njano.	
(vi)	Baada ya kuchomoza kwa jua kiasi cha mita tatu hadi kabla ya jua kufika kati kati.	

SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Orodhesha tofauti sita baina ya malaika na wanadamu.

4. (a) Kwa kutumia hoja tatu, bainisha udhaifu wa madai kuwa Mahari inashusha hadhi ya mwanamke.

   (b) Toa sababu tatu za mwanamke wa Kiislamu aliyefiwa na mumewe kukaa Eda.

5. (a) Tathmini faida tatu walizopata Waislamu baada ya matokeo ya vita ya Badr.
   (b) Linganisha vitimbi vitatu vya wanafiki wa Madina walivyomfanyia Mtume Muhammad (S.A.W) na vile wanavyofanyiwa Waislamu wa leo.

6. (a) Bainisha lengo la kuumbwa kwa mwanadamu.
   (b) Kwa kutumia hoja mbili, onesha tofauti kati ya mwanadamu na mnyama.

7. Tumia hoja mbili kufafanua mgawanyo wa haki za Mwenyezi Mungu (S.W) kwa mujibu wa uislamu.

8. Chambua ishara tatu zilizowaongoza Waislamu kumchagua Abubakar (R.A) kuwa Khalifa wa kwanza baada ya kutawafu Mtume (S.AW).

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** katika sehemu hii.

9. Bainisha changamoto nne zinazosababisha kutoonekana kwa matokeo ya ibada ya Hijja.

10. Fafanua vigezo vinne vinavyotumika kubaini tofauti kati ya sura za Quran zilizoteremshwa Madinah?

11. Miongoni mwa upotofu wa wazi katika Dini ya Uislamu ni kukataa nafasi ya Hadithi za Mtume (S.A.W) kama msingi mkuu wa sheria. Bainisha udhaifu wa hoja tatu za wapinzani wa msingi huo.